Volume 10 Number 2, 2016

Special Edition

# CHEMCHEMI

## International Journal of Humanities and Social Sciences

ISBN 1563-1028

# MCHANGO WA JAMII YA WAESHA KATIKA KUENDELEZA LUGHA NA FASIHI YA KISWAHILI

**Pamela Yalwala Ngugi**

## Abstract

The Asian people arrived in Africa more than one hundred years ago from Pakistan and India. Many of them are the children of the generations that entered Kenya at the beginning of the twentieth century. They came in as merchants from Gujarati, railway workers from Punjabi and clerks from Goa. When they arrived in Kenya, they found very few Africans who understood English. So they had to use Kiswahili, a language which by then had become largely a means of communication with Africans, who were mostly domestic servants and workers in their stores. Due to this interaction, this community has contributed significantly to the language repertoire of Kenya at various levels including sociolinguistic language and literature. The aim of this article is to highlight the contribution of the Asian community in the field of sociolinguists, language and literature to the Kenyan community and East Africa at large.

**Keywords**: Contribution, sociolinguists, language, literature.

## Utangulizi

Hali nzuri ya anga pamoja na ukarimu wa Waswahili iliwezesha maingiliano mengi katika eneo la Pwani ambayo yaliibua mtagusano wa wanajamii kutoka maeneo mbalimbali duniani kama vile Uarabuni, Ureno, Ujerumani, Uingereza na Asia . Uhusiano huu ulianza takribani zaidi ya miaka mia moja iliyopita na ungalipo \ hadi sasa. Miongoni mwa wageni waliosafiri kuja huku ni Waasia. Jamii hii ya Waasia hujulikana kama Wahindi miongoni mwa jamii zingine za Afrika Mashariki. Hii haimaanishi kuwa Waasia wanazungumza lugha moja tu ya Kihindi, lakini, kama jamii, wao ni wanawingi lugha, (Lodhi, 2008 uk 3).

Kwa mujibu wa Lodhi (2008 uk 1) wakati Ibn Batuta alipozuru eneo la Afrika mashariki mnamo mwaka 1331 alipata kuwa utamaduni ulioegemea kwa Uislamu pamoja na Uafrika au Uesha \ ulikuwepo . Anataja kuwepo kwa elementi fulani za kiisimu na kitamaduni zilizo na misingi yake katika jamii ya Wahindi ambazo zinapatikana katika jamii ya kisasa ya Waswahili kama vile **tambuu** (*betel leaves*) na **popoo** (*areca nuts*). Kwa upande mwingine, msafiri Al Idrisi anatoa ripoti kuhusu

makazi ya Wahindi katika mto Zambezi mnamo AD 1150. Lodhi (2008 uk 1) anasema kuwa, wakati Vasco da Gama alipowasili Afrika Mashariki mwaka wa 1498, palikuwa na idadi kubwa ya Wahindi, kwa mfano palikuwa na rubani wa Kihindi aliyejulikana kwa lugha ya Kicutchi kama Mālam < Kiarabu 'mualim', maalim na sasa mwalimu. Rubani huyu aliwasafirisha Wareno kutoka Malindi hadi bandari ya Kalikat kule India.

Jamii ya sasa ya Waasia ina mizizi yake kwa wafanyikazi waliofika humu nchini kwenye karne ya kumi na tisa hasa mwaka wa 1895 ambao waliletwa na koloni la Uingereza ili kujenga reli ya kutoka Mombasa hadi Uganda na vilevile kupanda mmea wa sukari (Mbaabu 1985 uk 40). Wengine walikuja kama manahodha, wafanyi biashara, askari, wawekezaji, mafundisanifu, watawala na hata madaktari, wahandisi, mawakili na pia wakulima.

Kwa mujibu wa Neale (1974) kundi hili la Waasia hutumia lugha nyingi ambazo si rahisi kubainika. Kwa mujibu wa Lodhi (2008 uk 5) taipolojia ya lugha miongoni mwa Waeṣha ni kama ifuatayo:

a. Lugha ya Kimaeneo ya Ki-indic (*Indo- Aryan*) lugha ambayo hutumika nyumbani pamoja na matumizi ya Kiswahili.
b. Lugha za kijadi (*Classical languages*) ambapo tunapata matumizi ya Kiarabu, Kiajemi
   Kisanskrit kama lugha za ibada na sala za kidini.
c. Lugha rasmi kama vile Kigujarati, Kiurdu na Kihindi ambazo hutumika kama lugha ya
   kufunzia na mawasiliano ya kirasmi.

Waasia hawa walipowasili nchini, walipata Kiswahili kikiwa kiungo mwafaka cha mawasiliano. Uwezo wa lugha hii kama lugha ya mawasiliano ulikuwa umetambuliwa na watu kama Kraph na Rebmann, wamishenari waasisi ambao walianza kushughulikia utayarishaji wa kamusi ya Kiswahili ili iwasaidie watu kujenga na kuendeleza msamiati wa lugha hii ambayo waliitilia maanani. Hivyo basi, lugha hii ndiyo iliyotumika kama lugha ya mawasiliano miongoni mwa Waesha na Waafrika ambao wengi wao hawakufahamu Kiingereza. Wengi wa Waafrika hawa walikuwa wameajiriwa na Waasha kama watumishi wa nyumbani au wafanyikazi katika maduka yao. Ni katika muktadha huu ambapo makala haya yanahoji kuwa jamii ya Waasia imechangia katika taaluma ya isimujamii na katika kuendeleza Kiswahili kwa upande wa msamiati tangu palipozuka uhusiano kati ya Wakenya na Waasia.

**Mtagusano wa Lugha ya Kiswahili na Lugha za Waasia**

Mekacha (2011 uk 108) aanaeleza kuwa kuanzia karne ya 7 hadi kufikia mwanzoni mwa karne ya 19, matumizi ya Kiswahili yalizidi kupanuka na kuimarika kama lugha ya biashara na lugha ya dini \ katika maeneo ya pwani na visiwa vya Bahari Hindi, ambako tayari kulikuwa na miji na vituo vikubwa vya biashara na utawala. Kutokana na dhima hizo, lugha hii ilitumika katika mawasiliano mapana miongoni mwa jamii za watu waliozungumza lugha tofauti. Katika misafara yao kwenda na kurejea kutoka bara kupitia katika vituo, maeneo na njia maalum, wafanyabiashara hao walitumia Kiswahili \. Njia na vituo ilimopitia misafara hiyo ilikuwa kama mtandao wa mishipa ya kueneza Kiswahili katika maeneo mengi ya Afrika Mashariki na Kati.

Tangu enzi hizo Kiswahili kilianza kukabiliana na lugha nyingine za bara na za kigeni. Wakati huo jamiilugha ya Waswahili ilikuwa imegawanyika katika makundi mawili; kundi la watumiaji wa Kiswahili kama lugha ya awali katika maeneo ya pwani na visiwa vya Bahari ya Hindi, na kundi la watumiaji wa Kiswahili kama lugha ya biashara, dini na uhusiano wa kijamii. Katika kundi la kwanza, Kiswahili kinachukuliwa kama lugha ya kwanza ya wasemaji wake na ambayo imekuwa hivyo tangu zamani. Kimsingi, Kiswahili kilikuwa na takribani lahaja kumi na tano zinazozungumzwa katika upwa wa Afrika Mashariki na visiwa vya Bahari Hindi na jamii za Waswahili.

Katika kundi la pili, Kiswahili kinachukua nafasi, dhima na uamilifu wa lugha ya jamii pana inayovuka mipaka ya kimaeneo, kitamaduni na kikabila. Haya ni matumizi ya Kiswahili ambayo yanatofautiana kimsingi na yale ya jamii za makabila ya Kiswahili. Ni matumizi ya lugha yaliyofungamana na lugha ya Kiswahili kama lugha ya awali, lakini ambayo hayafungamani na utamaduni wa jamii zinazokaa maeneo ya pwani na wala hayafungamani na utamaduni wa dini ya Kiislamu (Mekacha, 2011 uk 31). Haya ni matumizi ya lugha ya Kiswahili yatokanayo na nafasi, dhima na uamilifu wake kama lugha ya mawasiliano mapana katika jamii. Hivyo basi inakuwa kama kielelezo cha shughuli zote za kijamii na kitamaduni zinazovuka mipaka ya jamii za kikabila na kuhusishwa na, au kukubalika kama shughuli za jamii pana na isiyo ya kikabila. Kundi hili la wanajamii huwa na lugha zao za kwanza wanazozitumia katika shughuli zao wenyewe.

Katika hali hii panazuka mwingiliano mkubwa wa matumizi ya lugha hizi katika viwango mbalimbali vya kiisimu. Mwingiliano huu huzua vilauni vya lugha. Katika kurejelea Kiswahili, Munyua (2002 uk 98) anaziita aina hizi za vilugha "Viswahili" vya Kiswahili, kwa sababu hazijibainishi kama mojawapo wa lahaja za

Kiswahili. "Viswahili" hivi visivyobainika hutokea kutokana na wazungumzaji wa Kiswahili kutoka makabila tofauti tofauti wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya pili, (Munyua, 2002 uk 97; Kitonga, 2005 uk 4). Massamba, Kihore na Msanjila (2004 uk 10) wanaita hali hii lafudhi. Wanahoji kuwa lafudhi ni sifa ya kimasikizi ya mtu binafsi ambayo humpa msemaji \ utambulisho fulani ama wa jamii au wa kieneo. Tofauti hii ya uzungumzi wa Kiswahili inatokana na athari za lugha zao za kwanza. Hii ina maana kuwa watu wanapokizungumza Kiswahili wanakizungumza kama wanavyozungumza lugha yao ya kwanza. Kitonga (2005) anadai kuwa sifa mojawapo ya launi hizi ni ugeuzaji wa sarufi katika Kiswahili sanifu. Ugeuzaji huu hujitokeza katika viwango vyote vya isimu kama vile fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki. Launi hii ya Kiswahili haibainiki tu kwa Wakenya wanaozungumza lugha mbalimbali, bali inabaika pia miongoni mwa jamii ya Waasia wanapowasiliana na Wakenya wa maeneo mbalimbali. Kiswahili wanachotumia Waesha huwa kimeathiriwa na lugha zao mbalimbali.

Asili ya kundi la Waesha ni bara la Asia ambapo panapatikana nchi 48 zilizo na watu wanaozungumza lugha tofauti tofauti. Kwa mujibu wa Neale (1974) Waesha wanaoishi nchini Kenya wanaweza kugawanywa katika makundi matatu ya kikabila kulingana na asili yao: Wagujarati (70%), Wapunjabi (20 %) na Wagoa (10%) pamoja na idadi nyingine ndogo kama Wasandhi, Wamarathis na Wabengali. Kimsingi Waesha wengi hujitambulisha kuwa \ Wahindi wa Kaskazini. Nao hutumia lugha nyingi za kiasili kama vile Kihindi, \, Kigoa, Kigujarati, Kibengali, Kicutchi, Konkani na hata Kiarabu. Lugha hizi zina asili yake katika lugha ya Kisanskriti.

Kijamii, Waesha tofauti tofauti hutumia ishara fulani kama kitambulisho cha kuonyesha tofauti yao. Ruwaza za tofauti hizi huhusishwa \ na nembo za utamaduni kama vile kilemba kinachovaliwa na Wasikh wa Namdharia na kilemba kilichochogoka kwa Wasikh \ wengineo. Tofauti zingine ni kama vile majina, mavazi, vyakula na ndoa ( Kitonga, 2005 uk 4) .

**Matumizi ya Launi ya Kiswahili chaWaesha**

Ili Waesha waweze kuwasiliana na wenyeji, ilibidi wajifunze Kiswahili. Katika kujifunza Kiswahili walizua matumizi mapya pamoja na kupanua msamiati wa lugha \ yao. Hivyo basi kijilugha hiki walichokizua kinakidhi dhima na uamilifu katika jamii hii ya Waesha. Dhana muhimu katika mchakato huu ni "Maeneo ya matumizi ya lugha', (Mekacha 2011 uk 49). Dhana hii inahusu muktadha halisi wa kijamii wa matumizi ya lugha. Muktadha huu unatokana na kuhusisha shughuli zinazofanywa na jamii inayohusika, mada za mazungumzo, uhusiano miongoni mwa

wanaowasiliana na mahali kunapofanyika mawasiliano hayo.Katika muktadha wa kiisimujamii tunaweza kutaja kuwa kufahamu ni lugha ipi inatazamiwa kutumika katika eneo gani ni kufahamu mojawapo ya kanuni muhimu za kiisimujamii katika jamiilugha husika.

Kwa mujibu wa Mbaabu (1987 uk 7) Kiswahili kina irabu tano / a/ ɛ/ /i / ɔ/, /u /. Irabu hizi hupatikana kama silabi, viishio vya silabi au katika mwisho wa maneno. Kwa upande mwingine idadi ya konsonanti katika lugha ya Kiswahili ni kubwa zaidi ikilinganishwa na irabu. Konsonanti hizi ni: [p], [t], [tʃ], [k], [f], [Θ], [s],[ʃ], [kh],[m], [n], [w],[l],[b],[d], [dz],[g], [v/],[ð],[ z], [ɣ],[h], [n],[ŋ], [y] [r], [j]. Kunazo pia konsonanti zinazoambatana na zingine kama vile [nj],[ mb]na [nd].
Kitonga (2005 uk 35) anahoji kuwa Waesha wamedumisha kitengo fulani cha utamaduni kwa namna fulani ya usimilishwaji au uigaji teule, kwa kukopa yale wanayohitaji kutoka kwa wengine na kuyafanya yao. Waesha hawa wamesimilisha Kiswahili na kukibadilisha kwa kuweka athari fulani na papo hapo kuibusha launi ya Kiswahili ambayo ni tofauti na Kiswahili sanifu au hata ``viswahili`` vingine vinavyozungumzwa na wanajamii wengine.

Katika kuchanganua upekee wa Kiswahili cha Waesha, mtafiti alitembelea soko la City Market na maduka yanayomilikiwa na Waesha na hata mtaa wa Parklands wanakoishi Waasia wengi katika jiji la Nairobi nchini Kenya ili kupata data. Mazungumzo kati ya Waesha na wafanyikazi wengine kutoka maeneo mbalimbali ya nchi ya Kenya yalisikilizwa na kurekodiwa kwa makini kisha kuchanganuliwa katika awamu ya kwanza ya utafiti. Awami ya pili ya kupata mchango wa Waesha kwa fasihi ilitokana na utafiti wa maktabani na kwenye mtandao ambapo vitabu kuhusu historia ya Waesha katika nchi ya Kenya vilisomwa.

## Tofauti katika Kiwango cha Fonolojia

Kwa mujibu wa Naele (1974) na Kitonga (2005) launi ya Kiswahili ya Waesha ina konsonanti 19 ambazo ni [p], [b], [t], [d], [k], [g] , [ʧ ], [ j], [f],[v], [ h], [s] , [z], [ʃ] , [ m] , [ n] [ŋ], [ l], [r], na vokali 5 ambazo ni /I /, / ἐ/ , / a/, / ɔ/, /u /. Vikwamizwa vitatu vya Kiswahili sanifu /Θ/ /ð/, / ɣ/ havipo katika launi hii.
Waesha huweza kuingiza mabadiliko mengi ya kifonolojia katika Kiswahili na hivyo basi mpangilio wa vitamkwa kuunda silabi na kanuni mbalimbali za kujenga maneno huibuka kwa njia tofauti.

1. Katika launi ya Waesha sauti /Θ/ hubadilika na kuwa /s/.

Θɛna ʃara → sena ʃara

2. Katika launi ya Kiswahili cha Waesha, Sauti / ŋ/ haitokei mwanzoni mwa neno, badala yake /g/ hutanguliza maneno.

   Kwa mfano; ŋ→g

   ŋɔmbɛ → gɔmbɛ

3. Sauti /w/ huwa haijitokezi katika neno iwapo inafuata konsonanti hivyo basi w huwa kapa.

   Kwa mfano: w → Θ

   Mwaka →*maka*

   Bwana → *bana*

   Mwezi →*mezi*

4. Waesha hudondosha irabu iwapo zimetangulia konsonanti

   Kwa mfano: V→Θ—/ K

   Asubuhi → Θ *subui*

   Iʃirini → Θ *ʃirini*

   Ilikuwa → Θ *likuwa*

5. Waesha hudondosha sauti /w/ na mahali pake wanaweka /v/

   Wewe → *vɛvɛ*

   Watu → *vatu*

   Wali → *vali*

   *Miwa* → *miva*

## Kiwango cha Mofolojia

Maneno ya Kiswahili yaliyoasilia huwa yanafuata utaratibu wa viambishi na mizizi. Viambisihi hivi vinaweza kuwa mwishoni mwa mzizi au vinaweza kutangulia mzizi (Massamba na wengine 2004). Launi ya Kiswahili cha Waesha hukwepa utaratibu huu wa viambishi na mzizi na kila mzungunzaji hutumia mbinu zake mwenyewe anazofikiria kuwa zitamsaidia kufikisha ujumbe.

| Kiswahili sanifu | Launi ya Kiswahili cha Waesha |
|---|---|
| mtoto | *Toto wingi* |
| nitaenda | *Taenda* |
| ilikuwa | *Likuwa* |
| ataona | *Taona* |

Viambishi awali katika **mtoto, nitaenda** na **ilikuwa** vimedondoshwa na kuanza kwa mizizi. Neno '**watoto**' ambalo huchukuwa **wa**- kama kiambishi wingi huwa *matoto* katika Kiswahili cha Waesha. Hii ina maana kuwa kiambishi 'wa'- hugeuzwa na kuwa 'ma'- katika wingi.
Baadhi ya viambisihi awali vya wakati uliopita huondolewa na badala ya viwakilishi nomino kama vile mimi au sisi hutumika

| Kiswahili Sanifu | Launi ya Waesha |
|---|---|
| Tuliwaona | *Sisi au mimi naona* |
| Hatukulala | *Sisi apana lala* |
| Ninaenda huko | *Mimi nakwenda huko* |

Katika Kiswahili mofimu {ni} hutumika kwa maana mbili, kwanza kuonysha wingi na pili kuonyesha "ndani ya". Hata hivyo Waesha wanapotumia {ni} ili kuonysha 'ndani ya' huitumia kimakosa kwa kuirudufisha hali hiyo. Kwa mfano:

| Kiswahili Sanifu | Kiswahili cha Waesha |
|---|---|
| Ndani ya nyumba | *Ndani ya nyumbani* |

Katika enzi za ukoloni jamii ya Waesha ilijitenga na jamii zingine zote kwa misingi ya kijamii na hata kiuchumi kwa mujibu wa sheria za kikoloni zilizowekwa Hivyo basi hapakuwa na juhudi zozote zilizofanywa ili kuweza kuyarekebisha matumizi yao ya lugha. Hata hivyo, hivi karibuni jamii hii imeanza kutagusana na wanajamii wengine katika viwango vya kijamii, kisiasa na hata kiuchumi. Kwa mfano, wapo Waesha wanaowania uongozi katika maeneo ambayo ni ya watu wa kabila tofauti kama vile Wameru na Waluo. Vile vile watoto wengi wa Kiesha huhudhuria shule zilizo na wazungumzaji kutoka maeneo tofauti ya Kenya. Hivyo basi wengi wanajaribu kujifunza Kiswahili ili wasihusishwe na launi ambayo imewatambulisha kwa muda mrefu.

## Mchango wa Jamii ya Kihindi katika Kuendeleza Fasihi na Msamiati wa Kiswahili

Panapokuwa na mtagusano wa lugha, hapakosi hali ya kukopa maneno pande zote au hata upande mmoja tu wa jamii. Hali hii inabainika katika mtagusano wa lugha za Waesha na Kiswahili. Lodhi (2008 uk 7) anadai kuwa maneno mengi kutoka lugha za Kihindi yaliingizwa katika Kiswahili hata kabla ya kuja kwa Wareno Afrika Mashariki mnamo mwaka wa 1498. Hii ni kwa sababu kulikuwa na takribani Wahindi wengi waliokuwa wanaishi sehemu za pwani. Aidha, katika miaka ya 1700, Wahindi wengi walikuwa wameajiriwa na Wareno katika kikosi chao.

Baada ya ufalme wa Ki-Omani kuvamia na kunyakua pwani ya Afrika Mashariki kuanzia miaka ya 1821 na kuufanya mji wa Zanzibar kuwa makao yake makuu, jamii ya Wahindi ilianza kuongezeka na kuenziwa. Mfalme Seyyid Said alihimiza uhusiano na Wahindi na akawa anafanya biashara nao ya misafara na hata kuwafanya kuwa wafanyakazi wa bandari. Baadhi ya Wahindi waliotangulia Afrika Mashariki hata kabla ya kuja kwa Wareno ni Musa Mzuri wa Tabora (1825) na Alidina Visram wa Kampala (1896).

Kwa mujibu wa Lodhi (2008), ni Waesha wachache sana wanaochangia katika uandishi wa mashairi na hakuna yeyote aliyeandika riwaya ya Kiswahili. Hata hivyo, inabainika kuwa kufikia mwisho wa karne ya 19 na mwanzo wa karne ya ishirini, kulikuwa na mchango mdogo sana katika kazi za kiusomi Afrika Mashariki kutoka kwa Waesha. Baadhi ya kazi hizo chache ni kazi ya Alidina Somjee Lilani mzungumzaji wa Ki-Cutchi aliyeandika sarufi ya Kiswahili kwa lugha ya Gujarati mnamo mwaka wa 1890. Vilevile katika mwaka wa 1911, familia ya Jivanjee ilimpa kazi Dr. A. Attani aliyekuwa mzungumzaji wa Kigujarati kuandika Historia ya Zanzibar .

Lodhi (2008) anasema kuwa kabla ya Vita Vikuu vya pili vya Ulimwengu vya 1935 palikuwa na watunzi wachache wa Kiasia waliotunga mashairi na nyimbo. Hawa ni pamoja na Ustaad Ismail Raghi wa Tanga, na mpwa wake Ustaadh Mitu (kwa jina lingine Ayoub Ahmed Ayoub Rangooni) wa Zanzibar/Dar es salaam na Ustaadh Mohamoud Rajab Damodar wa Ndagoni, katika Kisiwa cha Mafia. Ingawa mashairi na nyimbo za watunzi hawa hazikuhifadhiwa, nyimbo chache na mashairi yanapatikana. Kwa mfano, katika mashairi na nyimbo za Raghi, wimbo mmoja wa Ustaadh Mitu,unaojulikana kama "Baba Pakistan", ni baadhi ya tungo zilizorekodiwa na 'Umm Kulthum' wa Afrika Mashariki. Wimbo wa "Baba Pakistan" uliimbwa sana na mwimbaji Siti binti Saad katika miaka ya 1940. Hivi majuzi wimbo huu

umerekodiwa kwenye video na Bi. Kidude (Fatuma binti Baraka) kule Zanzibar. Shairi moja la Damodar linalojulikana kama "Sabasaba 1964" lilihifadhiwa na Saadani Abdul Kandoro, katika mkusanyiko wa Mashairi yake (Kandoro, 1972).

Kandoro (1972) anaeleza kuwa, baadhi ya watunzi na waandishi wengine wa kisasa ni pamoja na Ustadh Ahmad Nassir Juma Bhalo wa Mombasa (babu yake alikuwa ni Mucutchi wa Badala) pamoja na binamu wake ambaye ni mwimbaji, Ustadhi Mohamed Bhalo ambaye usuli wake ni mchanganyiko wa Cutchi-Gujarati-Uarabu na Uafrika. Naye Ahmed Nassir alichapisha mkusanyika wa mashairiha mwaka wa 1966 pamoja na makala mbalimbali na nyimbo za Taarabu. Ikumbukwe kuwa nyimbo za taarabu zina athari yake katika filamu kutoka Cairo, Beirut na Bombay. Baadhi ya nyimbo hizi ni tafsiri kutoka Kihindi.

Kwa mujibu wa Lodhi (2008) mnamo mwaka wa 1955 kule Mombasa, mwalimu mmoja Bw. B. V. Trivedi, mzungumzaji wa Kigujarati (ambaye ni Mhindi) alichapisha kamusi ya Kigujarati - Kiswahili. Naye Dkt. Farouk Topan ambaye usuli wake ni mchanganyiko wa Cutchi-Gujarati-Uarabu na Uafrika, aliyeishi London na ambaye familia yake ilitokana na ile ya Tharia Topan ya Zanzibar alihariri mikusanyiko miwili ya mashairi yaliyolenga Azimio la Arusha, na *Arusha Declaration.* Vilevile katika mwaka wa 1971 na 1973 mtawalia, Farouk Topan aliandika tamthilia mbili za kidhihaki katika Kiswahili, *Mfalme Juha (1971) na Aliyeonja Pepo (1973)* . Tamthilia ya *Mfalme Juha* (1971) ni usimilisho wa shairi "Andheri Nagari Gandu Rajah" la Kigujarati lililoandikwa katika karne ya 13. Topan alichangia sana katika masuala mengi ya kiusomi ya Kiswahili kwa kuandika makala mbalimbali. Muhimu zaidi, yeye ndiye aliyekuwa mwanzilishi wa taaluma ya Fasihi ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwishoni mwa mwaka wa 1960. Katika mwaka wa 1968, Abdulaziz Y. Lodhi alichapisha kusanyiko moja la mashairi lijulikanalo kama *Tafkira*, (1968) katika Kiswahili, na mashairi mengine mengi katika majarida ya Kiswahili, makamusi na makala mbalimbali ya kiisimu kuhusiana na Kiswahili. Usuli wake ni wa ukoo wa Pathan-Baluch-Cutchi-Sindhi-Burmese.

Wataalumu wengine wa asili ya Kiesha ni pamoja na Maalim Jaafer Tejani wa kutoka Zanzibar. Tejani alikuwa mkurugenzi wa kwanza wa Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili huko Dar es Salaamu. Usuli wake kiukoo ni wa Kicutchi na Kiajemi. Katika miaka ya 1950 na 1960 palikuwa na mtaalamu mmoja wa Kiswahili aliyejulikana kama Ibrahim Sardar wa usuli wa WaCutchi wa ukoo wa Sameja. Sardar alikuwa mkuu wa idara ya Kiswahili katika shule ya Sekondari ya Aga Khan kule Dar es Salaamu.

Kaimu wake alikuwa \ Mohamed Kamal Khan aliyekuwa Mbalochi. Vitabu vyake vilitumika sana katika shule za sekondari.

**Mchango wa Lugha za Kiesha katika Msamiati wa Kiswahili**

Kwa mujibu wa Lodhi (2008 uk 9) maneno mengi yaliyokopwa kutoka kwa lugha za Kiasia yalitokana na lugha ya Kicutchi. Lodhi ametoa orodha ya maneno ya Kiasia ambayo yamekuwa yakitumika katika Kiswahili. Maneno haya yamechangia katika kukuza Kiswahili na hata lugha nyinginezo za Kiafrika.

**Maneno ya mkopo**

| Kiswahili | Kicutchi | Kigujarati | Kiingereza |
|---|---|---|---|
| Bangili | Bangle | bangadibangle | armlet |
| Biri | bīrī | bīdī | cigarette |
| Bofu | Fōfilō | Fōfulo | baloon |
| Chamburo | Čāmpro | Čāmpdo | tongs |
| Fataki | Fatāki | Fatākio, fatakdo | fireworks |
| Gunia | Guni | Gūṇ | sack |
| Sukari | Guru | Gōr | Brown raw sugar |
| Jaribosi | Jarpōs | Zari | tinfoil |
| Nanga | Nangar | Langar | anchor |
| Ndimu | līmū | Limbu | lemon |
| Sonara | Sonārā | sōnī | goldsmith |

Mbaabu (1995 uk 41) anatoa orodha ya maneno yaliyokopwa kutoka Kihindi ifuatayo: Chai, embe, papuri, fenesi, ladu, paipai, pipa, pata, cheti, bebeeru, gari, godoro, gunia na terafini.

**Lawama za Kujitenga kwa Jamii ya Waesha**

Kwa muda mrefu jamii ya Waesha imechukuliwa kama jamii iliyojitenga na wanajamii wengine. Hali hii inaweza kuelezwa kupitia hali mbili tofauti. Kwanza, jamii ya Waesha ni jamii iliyojengeka kwenye misigi ya matabaka mbalimbali. Pili, wanajamii hawa walipowasili nchini Kenya nyakati za ukoloni walipata kuwa wakoloni tayari walikuwa wameweka misingi ya ubaguzi. Hivyo basi, wanajamii hawa waliruhusiwa kujitenga na tawala za koloni katika masuala ya kijamii. Wao walikuwa na shule zao maalumu na walichukuwa ngazi ya pili baada ya Wazungu kijamii (Bongoko, 1992 uk 2). Hata hivyo, Lodhi (2008 uk 4) anasema kuwa wapo wachache ambao walijitolea kupigania uhuru kama vile Makkhan Singh na Pio Gama Pinto katika miaka ya hamsini na sitini.

Baada ya uhuru hali hii iliendelea kuwa hivyo kwa muda mrefu. Ghai na Ghai (1965) wanasema kuwa katika harakati ya Wakenya kujinyakulia uhuru katika karne ya ishirini, Waesha wengi walihisi kutengwa na harakati ya mradi uliojulikana kama 'Utaifishaji wa nchi ya Kenya'. Mradi huu uligawa mashamba na kuwapa Wakenya kazi kubwa serikalini bila kujali Waesha walioshiriki katika kupigania ukombozi wa nchi. Vile vile, hatua ya aliyekuwa rais wa Uganda, Idi Amini ya kuwafurusha Waesha kutoka nchi hiyo katika mwaka wa 1972 iliwatia wasiwasi mwingi. Mwisho, hali ya kujitenga ilitokana na jaribio la kupindua serikali ya rais mstahaafu Daniel Moi lililofanyika mwaka wa 1982. Tukio hili liliwapelekea waesha wengi kupoteza mali nyingi kupitia kuporwa hasa katika maeneo ya sehemu za River Road ambao wengi wao waliendesha biashara zao. Huenda hali hizi ndizo zilizowafanya wengi wao kuhisi kuwa wangali wageni hata kama kikatiba ni Wakenya wa asiili ya Kiesha. Kutokana na fikra hizi wengi wao hawajashabikia Kiswahili kiasi cha kukimiliki, lugha ambayo ni ya taifa na lugha rasmi ya taifa la Kenya.

**Hitimisho**

Ingawa jamii ya Waesha inachukuliwa kuwa jamii funge, baadhi ya Waesha wamejitolea kujihusisha na masuala mbalimbali ya lugha na fasihi ya Kiswahili. Baadhi yao waliikubali lugha na kuifanya kuwa yao, wakaichangamkia na kuifanyia utafiti wa kina. Hivi sasa Waesha wengi wamechukua hatamu za uongozi kisiasa na matarajio ni kwamba watakienzi Kiswahili na hivyo basi kuwa vielelezo kwa wengine ambao bado hawajali namna wanavyotumia lugha hii

**Marejeleo**

Bogonko, S.N. (1992). *Reflections on Education in East Africa*. Nairobi: Oxford Univesity Press.

Ghai, D.P. & Ghai, Y.P. (1965). "Asians in East Africa: Problems and Prospects " katika The *Journal of Modern African Studies* Vol. 3, No. 1, Uk. 35-51.

Kandoro,S.A. (1972). *Mashairi ya Saadani*. Dar es Salaam: Mwananchi Publishing(1966) Limited.

Kitonga, N. N. (2005). Uswawazishaji wa Usmi kati ya Waasia na Waafrika katikati mwa jiji la Nairobi. Tasnifu ya Uzamili. Chuo cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Lodhi, A. Y. (2008). "Indians and Indic languages in Eastern Africa: The Status of South Asian Languages in Eastern Africa." Makala Karatasi iliyowasilishwa katika warsha kuhusu *Language Planning and Language Policies*, 4-6 Machi, 2008, Central Institute of Indian Languages (CIIL), Mysore, India.

Massamba, D.P.B. na Wenzake (2004). *Fonolojia ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI), Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam.

Mbaabu, I. (1985). *New Horizons in Kiswahili: A Synthesis in Developments, Research and Literature*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Mbaabu, I. (1987). *Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Kenya Publishing and Book Marketing Co. Ltd

Munyua, J, (2002) "The Emerging Viswahili and Kiswahili Research," Katika Inyani Simala (Mhr) *Utafiti wa Kiswahili*. Eldoret: Moi University Press. Uk. 97- 107.

Mekacha, R. D. K. (2011). *Isimujamii: Nadharia na Muktadha wa Kiswahili. Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.* Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Naele, B. (1974). "Kenya's Asian Language" Katika Whitley, W. (Mhr) *Language in Kenya*. Nairobi: Oxford University Press. Uk. 69-86.

Topan, F. (1971). *Mfalme Juha*. Dar es Salaam. Tanzania Publishing House.

Topan, F. (1973). *Aliyeonja Pepo*. Dar es Salaam. Tanzania Publishing House.

**About the Author**

Dr. Pamela Yalwala Ngugi is faculty in the Department of Kiswahili and African Languages, Kenyatta University.